## Mwongozo wa Kozi - Nyaraka za Paulo

# Kiini cha Theolojia ya Paulo.
# Nyaraka za Paulo akiwa gerezani

## MAELEZO YA KOZI

Paulo alitangaza kwa shauku habari njema ya wokovu wa mtu binafsi ndani ya Kristo Yesu. Lakini hii haikuwa kiini cha injili yake. Kulingana na Paulo, kimsingi wokovu hauhusiki na mtu kuokolewa kutoka katika ghadhabu ya Mungu tu, bali injili inahusu ushindi wa Yesu Kristo na Ufalme wa Mungu. Ujumbe mkuu katika Kozi hii unahusu ushindi wa Kristo na Ufalme wa Mungu, kama vile Paulo alivyoandika katika Wagalatia, 1&2Wathesalonike, na 1&2Wakorintho. Utapata uelewa mzuri wa ufalme wa Mungu na utafurahishwa na kushangazwa na mipango aliyo nayo Kristo Yesu kwa watu na ulimwengu wake. Wakati huohuo sisi wakristo tunakabiliana na changamoto nyingi katika maisha ya Imani yetu. Mafundisho ya uongo, na mitazamo ya ulimwengu huu hushambulia na kusonga uaminifu wetu kwa Kristo. Majaribu hutufanya kufikiri kuwa Mungu hana udhabiti au kwamba hana nia nzuri nasi. Uhusiano wetu na waumini wengine mara nyingine hukubwa na matatizo kiasi kwamba tunatilia shaka thamani ya Kanisa. Kupitia kozi hii utaona jinsi masuala haya na mengine yanavyojibiwa na Paulo katika nyaraka zake kwa Wakolosai, Waefeso, Filemoni, na Wafilipi. Kozi hii ni ya msingi katika mfululizo wa video za Kiini cha Theolojia ya Paulo na nyaraka zake za gerezani, imeandaliwa na Kutolewa na Third Millennium Ministries na kuwasilishwa na Dkt. Reggie M. Kidd.

## MALENGO NA MALENGO MAHUSUSI

### *Malengo*

Katika Kozi hii, tumelenga kukamilisha yafuatayo:

1. Ni matumaini yetu kwamba, utajifunza mafundisho haya muhimu kuhusu Paulo, asili yake na kiini cha Theolojia yake, tukizingatia barua yake kwa Wagalatia, Waefeso, Filemoni na Wafilipi.

2. Ni matumaini yetu kuwa, utajifunza na kufikia kiwango cha kufurahia neema ya Mungu na jumuiya ya Ufalme wake na kwamba utakuza mtazamo wako kuhusu mateso wakati wa sasa na ujio wa pili wa Kristo, na jinsi unavyoendana na mpango mkubwa zaidi ufalme wa Mungu.

3. Ni matumaini yetu kwamba, utatumia mafundisho ya nyaraka hizi za Agano Jipya katika maisha yako. Tuna Tumaini pia kuwa utashiriki kikamilifu katika upanuzi wa Ufalme wa Mungu wakati unangojea kurudi kwa Kristo, kwamba utakuwa mwaminifu zaidi katika mwenendo wako wa Kikristo. Ukijifunza kustahimili katikati ya mateso, utashughulikia

mafundisho ya uongo, uwezo wa kutatua migogoro, na kuwatia moyo wengine katika Kristo.

## MALENGO MAHUSUSI

**Ukikamilisha yafuatayo, utakuwa umefikia malengo;**

1. Ukipata alama za kuridhisha katika maswali yote na mitihani, kuonyesha kuwa unaelewa mafundisho muhimu ya Biblia kuhusu huduma ya Paulo, usuli na maudhui ya barua zake kwa Wagalatia, Wathesalonike, Wakorintho, Wakolosai, Filemoni na Wafilipi, na kwamba unaelewa mkazo mkuu wa Theolojia ya Paulo.

2. Utajadili nyenzo mbalimbali na kikundi chako ukieleza mtazamo wako kuhusu neema ya Mungu, jumuiya ya ufalme wa Mungu, ujio wa pili wa Kristo, na kuonyesha jinsi kozi hii inavyobadili maisha yako. Hasa unavyojifunza kuvumilia katikati ya Mateso, kushughulika na mafundisho ya Uongo, kutatua migogoro, na kuwatia moyo wengine katika Kristo Yesu.

## Orodha ya Moduli za Kozi ya Nyaraka za Paulo

1. Paulo, Theolojia yake, na Wagalatia
2. Paulo na Wathesalonike
3. Paulo na Wakorintho
4. Kifungo cha Pulo
5. Paulo na Wakolosai
6. Paulo na Waefeso
7. Paulo na Filemoni
8. Paulo na Wafilipi

## UFAFANUZI WA VIPENGELE VYA KOZI

### *Beji*

1. Kila wiki ya majadiliano katika kikundi, tenga muda kwa ajili ya kufanya kazi pamoja kufuatia maelekezo ya beji. Mwongozo huu wa kurasa mbili utatoa mwelekeo wa jumla kwa mkufunzi wako unapotafuta kukuza ujuzi huu muhimu wa huduma.
2. Katika wiki chache, sehemu ya muda wako wa majadiliano itatumika kupitia Mada za majadiliano zilizotolewa katika maagizo ya beji.
3. Ukishakuwa na msingi mzuri wa majadiliano ya kikundi, tumia wiki zilizobaki kufanya kazi ya Beji ya ***Wito kwa Vitendo***.
4. Utatunukiwa beji endapo Mkufunzi wako atakaporidhika kuwa umekamilisha hatua, kwa kuzingatia maelekezo ya hatua za vitendo za Beji.

### *Moduli*

1. Soma masomo, na kutazama **video,** sikiliza **sauti,** au Soma **nukuu za somo husika**.

2. Kamilisha **Miongozo ya Somo** kwa kila Moduli. Tumia Miongozo ya masomo kujitayarisha kwa ajili ya ***maswali ya majaribio.***
3. Fanya majaribio kwa njia ya mtandao kwa kila moduli. Unaweza kufanya Majaribio mara nyingi kwa kadri uwezavyo, lakini itakupasa kusubiri saa moja kabla ya kurudia jaribio hilo. Alama za juu utakazopata katika jaribio zitatumika rasmi. Tunashauri upate angalau 80% kabla ya kushiriki katika majadiliano ya kila wiki ili kuhakikisha kuwa unaelewa dhana kwa usahihi.
4. Shirikiana na wanakikundi wenzako katika *majadiliano* ya kila wiki, pamoja na mkufunzi wako, kwa kutumia ***Mwongozo na maswali ya kujadili***. Majadiliano ni muhimu kwa ajili ya kukuza ufahamu wako wa matumizi ya nyenzo za kozi, lakini pia yanakuza uwezo wako wa kutumia dhana kwa usahihi katika maisha na huduma yako. Tunapendekeza mjadala wa kila moduli udumu angalau saa moja.

***Mtihani wa Mwisho***

Unaweza kufanya mitihani mara nyingi kadiri uwezavyo, lakini ni lazima usubiri saa moja kwa kila mtihani. Daraja lenye alama za juu, ndilo litachukuliwa kuwa rasmi, ni sharti ufikie 80% au zaidi kwenye mtihani wa mwisho.

**DARAJA**

Daraja la Mtihani wa mwisho linahesabiwa kama ifuatavyo:

1. Maswali kwenye hotuba yana jumla ya alama 30.
2. Mtihani wa mwisho una alama 100.
3. Beji haitaathiri daraja lako, lakini lazima ikamilishwe kwa kuridhiwa na mkufunzi na iwekwe kwenye alama kuwa imekamilika katika orodha ya uhakiki wa mafunzo ya Biblia.

Ufaulu wa juu ni kuanzia 80%

------------------------------------

## Orodha ya wachangiaji katika kozi hii

**Dkt. David R. Bauer** ni Mtaaluma mkuu wa Shule ya Utafsiri wa Biblia na Profesa wa Ralph Waldo Beeson Professor of Inductive Biblical Studies kaika Seminari ya Asbury Theological.

**Dkt. Rick Boyd** ni Profesa wa Utafsiri wa Biblia katika Seminari ya Wesley Biblical.

**Dkt. Constantine R. Campbell** Profesa Mshiriki wa Agano la Kale shule ya Trinity Evangelical Divinity.

**Dkt. D.A. Carson** ni Profesa wa utafiti wa Agano la kale katika Shule ya New Testament at Trinity Evangelical Divinity na Mwanzilishi mwenza wa The Gospel Coalition.

**Dkt. Robert B. Chisholm, Jr.** Mwenyekiti wa Idara na Profesa wa Agano la Kale katika Seminari ya Dallas Theological.

**Dkt. Ashish Chrispal** ni Mkurugenzi wa Asia for the Overseas Council.

**Dkt. David Correa** ni Profesa Mshiriki katika Seminari ya San Pablo Theological Merida, Mexico, Mkurugenzi wa Next Institute Mexico. Pia ni Mchungaji wa kanisa la Presbyterian Iglesia Jesus huko Progreso.

**Dkt. Brandon D. Crowe** ni Profesa Mshiriki wa Agano Jipya katika chuo cha Westminster Theological Seminary.

**Ndugu. Sherif Atef Fahim** ni mwalimu katika Shule ya Theolojia iitwayo Alexandria huko Misri.

**Rev. Michael J. Glodo** ni Profesa mshiriki wa Masomo ya Biblia katika chuo cha Reformed Theological huko Orlando, Florida.

**Dkt. Douglas Gropp** ni Profesa mstafu wa Agano la Jipya na mtaaluma mwandamizi katika Seminari ya Redeemer.

**Dkt. James M. Hamilton** ni Profesa Mshiriki wa Theolojia ya Biblia katika seminari ya Southern Baptist Theological Seminary na mchungaji Mhubiri katika Kanisa la Kenwood Baptist Church.

**Dkt. Joel C. Hunter** I ni Mchungaji kiongozi wa Northland, A Church Distributed huko ongwood, FL.

**Mch. Clete Hux** ni Mkurugenzi na anahusika na maswala ya kiutamaduni katika Apologetics Resource Center in Birmingham, AL.

**Dkt. Thaddeus J. James, Jr.** ni Makamu Raisi wa Maswala ya Taaluma katika Seminari ya Birmingham Theological Seminary.

**Dkt. Mark A. Jennings** ni Profesa wa Agano la jipya katika Seminari ya Gordon-Conwell Theological Seminary.

**Ndugu. Bradley T. Johnson** ni Profesa katika Seminari ya Asbury Theological na mchungaji wa Wesley Chapel UMC huko Nicholasville, KY.

**Dkt. Dennis E. Johnson** ni Profesa wa Theolojia ya Vitendo katika Seminari ya Westminster Seminary California.

**Dkt. Jim Jordan** ni mkufunzi anayeandaa viongozi wa kufandisha wengine kimataifa (Training Leaders International).

**Dkt. Edward M. Keazirian** ni Profesa Msaidizi wa lugha ya kigiriki na Mkurugenzi wa Mpango wa Lugha ya Kigiriki katika Seminari ya Gordon-Conwell Theological.

**Dkt. Craig Keener** ni F.M. na Ada wa Thompson Chair of Biblical Studies huko Asbury Theological Seminary.

**Dkt. Daniel Kim** ni Mwalimu wa Agano la Kale katika Seminari ya Covenant Theological Seminary.

**Mch. Kevin Labby** ni Mchungaji kiongozi wakanisa liitwalo Willow Creek huko Winter Springs, FL.

**Dkt. Dan Lacich** Anatumika katika timu ya Wachungaji ya Northland, A Church Distributed, huko Orlando, FL.

**Dkt. Richard Lints** ni Profesa wa Theolojia na Makamu Raisi wa Maswala ya Kitaaluma katika Seminari ya Gordon-Conwell.

**Dkt. Robert MacEwen** ni Mkufunzi katika Masomo ya Biblia na Mkurugenzi wa Kitengo cha Chinese Theology katika shule ya East Asia School of Theology, huko Singapore.

**Dkt. Sean McDonough** ni Profesa wa Agano Jipya Gordon-Conwell Theological Seminary.

**Mch. Timothy Mountfort** ni mtaaluma mkuu katika Seminari ya Western China Covenant Theological Seminary.

**Dkt. Matthew Newkirk** ni Raisi na Profesa wa Agano la Kale katika Seminari Christ Bible Seminary huko Okazaki, Japani.

**Dkt. Jeffrey J. Niehaus** ni Profesa wa Agano la Kale kaika Seminari ya Gordon-Conwell Theologica.

**Dkt. Jason Oakes** ni Profesa Msaidizi wa katika kitengo cha Christian Thought katika Shule ya Theolojia ya Talbot.

**Dkt. Luis Orteza** ni Profesa wa Ushauri katika Seminari ya Birmingham Theological Seminary.

**Dkt. Grant R. Osborne** (1942-2018) alikuwa Profesa wa Agano Jipya katika Shule ya Trinity Evangelical Divinity School.

**Dkt. John Oswalt** Ni Profesa wa Agano la Kale katika Seminari ya Asbury Theological Seminary

**Dkt. Alvin Padilla** ni Mtaluma katika huduma ya Hispanic Ministries na ni Profesa wa Agano Jipya katika Gordon-Conwell Theological Seminary.

**Dkt. Jonathan T. Pennington** ni Profesa mshiriki wa Tafsiri ya Agano Jipya na Mkurugenzi wa Utafiti katika masomo ya Doctoral Katika Seminari ya Southern Baptist Theological.

**Dkt. Gregory R. Perry** ni Profesa Mshiriki wa Agano jipya na mkurugenzi wa Huduma ya Initiative katika Seminari ya Covenant Theological, St. Louis, MO.

**Yohanes Praptowarso, Ph.D.,** anatumika katika Seminari ya Batu Theological.

**Dkt. Clay Quarterman** alikuwa Raisi wa Seminari ya Evangelical Reformed huko Ukraine hadi alipostaafu mwaka 2019.

**Dkt. Scott Redd** ni Raisi wa Kampasi ya Seminari ya Reformed Theological Seminary huko WashingtonD.C. na Profesa Mshiriki wa Agano la Kale.

**Mch. Ric Rodeheaver** ni Mchungaji kiongozi katika kanisa la Community Church huko Laguna Hills kalifornia.

**Dkt. Mike Ross** ni mwalimu wa theolojia ya vitendo katika Seminari ya Reformed Theological, na alikuwa mchungaji kiongozi katika Kanisa liitwalo Christ Covenant Church huko Matthews, NC.

**Dkt. Brian D. Russell** ni Profesa wa Masomo ya Biblia na mtaluma wa shule ya huduma ya Urban katika chuo cha Seminari ya theolojia Asbury huko Orlando, FL.

**Dkt. Philip Ryken** ni Raisi wa chuo cha Wheaton.

**Dkt. Eckhard Schnabel** ni Profesa wa Agano jipya katika Seminari ya Gordon-Conwell Theological.

**Dkt. Glen Scorgie** ni Profesa wa Theolojia katika Seminari ya Bethel kampasi ya San Diego.

**Dkt. Daniel Simango** ni mkuu wa chuo kiitwacho The Bible Institute of South Africa huko Afrika kusini katika mji wa Cape Town.

**Dkt. Vuyani Sindo** ni Mkufunzi katika Chuo cha George Whitefield huko Afrika Kusini.

**Dkt. Daniel Steffen** ni Profesa mwalikwa katika Seminari ya Teológical Centroamericano katika Jiji la Guatemala.

**Dkt. Mark L. Strauss** ni profesa wa Agano jipya katika Seminari ya Bethel, San Diego.

**Dkt. Derek Thomas** ni Profesa wa Utaratibu na Historia ya Theolojia katika Seminari ya theolojia iliyorekebishwa huko Atlanta, GA.

**Mch. Dkt. Simon Vibert** ni wakili mstaafu wa Kanisa la Mt Luke's Church huko UK, na kwa sasa ni makamu mkuu wa Wycliffe Hall, Oxford, na Mkurugenzi wa shule ya Mahubiri.

**Dkt. Peter Walker** ametumika kama Profesa wa Masomo ya Biblia katika shule ya Trinity School for Ministry na Makamu mkuu wa Wycliffe Hall, Oxford. Kwa sasa ni mkufunzi katika kituo cha Kibiblia kiitwacho Yerusalem.

**Dkt. Stephen J. Wellum** ni Profesa wa Theolojia ya Kikristo katika Seminari ya Southern Baptist Theological Seminary.

**Dkt. Stephen E. Witmer** ni Profesa wa Agano Jipya katika Seminari ya Gordon-Conwell Theological.

**Dkt. Jonathan D. Worthington** ni Mkurugenzi wa ukuzaji wa mtaala katika Training Leaders International.